TANGAZO LA SERIKALI NA. 113 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA ILINDI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Ilindi ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama.

*Tangazo la Serikali na. 113 (linaendelea)*

________

JEDWALI

________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*
Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Mpaka unaanza kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 456052.63MS, 9573883.74KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ83$^{0}$08'22.34”MS kwa umbali wa kilomita2.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta458479.12MS, 9574175.36KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS2$^{0}$50'53.48”MG kwa umbali wa kilomita 2.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 458349.27MS, 9571562.71KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS89$^{0}$06'04.74”MG kwa umbali wa kilomita 2.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 456054.31MS, 9571526.76KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ0$^{0}$02'55.02”MG kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi ulipoanzia.”

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi,*
*Nyumba na Maendeleo ya Makazi*